# OFISI YA RAIS – TAMISEMI.
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI MNINGA,
S.L.P 2,
**MUFINDI.**
TAREHE: ……………………….

Kumb Na: MNSS/JNI/40/13
JINA LA MWANAFUNZI:……………………………….
S.L.P …………………….

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA KATIKA SHULE YA SEKONDARI MNINGA.**

## 1.0.UTANGULIZI

⇒ Napenda kuchukua nafasi hii kukupa HONGERA kwa kuchaguliwa kujiunga na KIDATO CHA KWANZA katika shule ya sekondari Mninga.

⇒ Shule hii ipo kata ya MNINGA.

⇒ Hali ya hewa ni ya baridi na ni nzuri sana kwa masomo.

## 2.0.KUFUNGUA SHULE

⇒ Shule itafunguliwa tarehe ……………………………… Na kila mwanafunzi anatakiwa afike shule siku hiyo bila kukosa akiwa na mahitaji yote ya shule kama ilivyoagizwa.

⇒ Shule ya sekondari Mninga ni shule ya kutwa na ni Shule ya mchanganyiko wavulana na wasichana.

## 3.0.MASOMO

⇒ Shule inafundisha masomo yafuatayo: Hisabati, Jiografia, Uraia, Historia, Kiswahili, Kiingereza, Biolojia, Fizikia, Kemia pamoja na somo la Dini ambapo kila mwanafunzi atahudhuria vipindi vya Dini yake.

## 4.0.SARE ZA SHULE

### 4.1.SARE YA SHULE WAVULANA

i. Suruali rangi nyeusi na rangi ya maruni (damu ya mzee) zilizoshonwa kwa heshima (zisizobana au modo)
ii. Mashati meupe mikono mirefu,
iii. Viatu vya ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi (Boots haziruhusiwi kabisa).
iv. Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi
v. Sweta jozi mbili (2) rangi ya Kijani jeshi.
vi. Tai rangi nyeusi na maruni
vii. Raba za michezo.
viii. Sare za michezo ni traki suti rangi ya bluu bahari.
ix. Begi la daftari.

**4.2.SARE YA SHULE WASICHANA**

i. Sketi rangi nyeusi na rangi ya maruni (damu ya mzee) zilizoshonwa kwa heshima (ndefu) unaweza kushona marinda au rinda box ya heshima.
ii. Mashati meupe mikono mirefu.
iii. Viatu vya ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi vyenye mkanda mmoja au viatu vya kamba.
iv. Soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe.
v. Sweta jozi mbili (2) rangi ya Kijani jeshi.
vi. Tai rangi nyeusi na maruni
vii. Raba za michezo.
viii. Sare za michezo ni traki suti rangi ya bluu bahari.
ix. Kwa atakaye vaa hijabu ni rangi nyeupe tu.
x. Begi la daftari.

**5.0.VIFAA VYINGINE VINAVYOHITAJIKA SHULENI.**

i. Cheti cha kuzaliwa
ii. Cheti cha afya kutoka kwa daktari (Kiambatanisho B)
iii. Daftari kubwa kumi (10) – (Counter Books 3Quire) ni lazima
iv. Mkebe pamoja na kalamu.

**6.0.SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu **Na. 25** ya mwaka **1978** na kama ilivyorekebishwa kwa sheria **Na. 10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yake inayotolewa na wizara ya elimu sayansi na teknolojia yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya **RAIS – TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingati ratiba ya shule wakati wote na kutunza mali za Umma.
i) Kila mwanafunzi itamlazimu kujifunza kujua wimbo wa shule, wimbo wa Taifa na Wimbo wa Tanzania nakupenda.
j) Kila mwanafunzi anapaswa kuhudhuria masomo yote kwa wakati uliopangwa bila kuchagua na bila kuchelewa.

**7.0.MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya, kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
g) Kudharau bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba.
i) Kutoa mimba.
j) Kusababisha mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

**8.0.MAELEKEZO MUHIMU**

a) Kila mzazi/mlezi inamlazimu kujaza kiambatanisho 'A' kwa ukamilifu na kuleta shuleni tarehe ya kufungua shule.
b) Kiambatanisho 'B' ni fomu ya kupima afya ya mwanafunzi, ijazwe baada ya kupimwa afya yake hospitalini na kuletwa shuleni tarehe ya kufungua shule.

**MWISHO**

1. Karibu Mninga Sekondari.
2. Shule yenye matumaini makubwa na maendeleo yako kitaaluma, kimichezo na kinidhamu.
3. Shule itakayokuandaa vyema kwa maisha yako bora ya baadaye.
4. Sheria za shule mwanafunzi atapewa afikapo shuleni.

......................................

**HADIJA YASSIN MADABI**
**MKUU WA SHULE.**
MAWASILIANO: 0766 031 910

KIAMBATANISHO 'A'

# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

________________________

________________________

________________________

TAREHE_________________

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MNINGA,
S.L.P 02,
**MUFINDI.**

**YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MNINGA.**

MWANAFUNZI: ___________________________________________________________
KIDATO: _____________________________ MWAKA: ______________________________

1. Mimi _____________________________________________________________
   Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu ninakiri kuwa nimeelewa maelezo yote yaliyotolewa na masharti ya fomu hii.
2. Nakubali mwanangu ajiunge na shule hii na nitatekeleza yale yote yanayonihusu kwa wakati wake kama ilivyoagizwa kwenye maelezo ya kujiunga na shule.
3. Ninaahidi kumuhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufanikisha malengo yake ya kujiunga na shule hii _________________________________.
4. Ninaahidi kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo shuleni.

JINA LA MZAZI/MLEZI:_____________________________ SAHIHI:__________________
ANUANI YA MZAZI/MLEZI: ___________________________________________________
NAMBA YA SIMU: _____________________________________________________________

Mimi ______________________________________________________________________
niliyechaguliwa kujiunga na shule hii, ninaahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kuwa na nidhamu ya kujituma, kusoma kwa bidii na kuwa mfano bora kwa wanafunzi wenzangu ili nifikie malengo ya shule hii. Tofauti na haya niondolewe shuleni mara moja.

JINA LA MWANAFUNZI: _____________________________________________________
SAHIHI: ___________________________________________________________________
TAREHE: __________________________________________________________________

KIAMBATANISHO 'B'

# MUFINDI DISTRICT COUNCIL

MNINGA SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 2,
**MUFINDI.**
DATE:..............................

**TO THE MEDICAL OFFICER**
....................................
....................................
....................................

## PART 'A'
## MEDICAL EXAMINATION

Name of student .................................... Please examine the above named student as to his/her physical and mental fitness for a full time student in this school.

**The examination should include the following categories:-**

1. Hemoglobin ..........................................................
2. P.V. Bleeding ..........................................................
3. Sight ..........................................................
4. Blood Pressure ..........................................................
5. Urine for sugar and pregnancy test ..........................................................
6. Stool for routine examination ..........................................................
7. Asthma ..........................................................
8. Skin disease ..........................................................
9. Leprosy ..........................................................
10. Any deformity ..........................................................
11. Epilepsy ..........................................................
12. Pulmonary tuberculosis ..........................................................
13. Neurosis ..........................................................
14. STDS ..........................................................
15. Other Serious diseases ..........................................................

## PART 'B'
## MEDICAL EXAMINATION
**(To be completed by a government medical officer)**

1. I have examined the above named student and consider that he/she is physically fit/and mentally fit for full time schooling.
2. Other comments: ..........................................................
..........................................................
3. Date : .......................................... Signature ..........................................

Title .......................................... Official Stamp..........................